# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

**FAHARI YA SAME**

*Maendeleo Daima*

***Toleo la Desemba 2023 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***

# WIZARA YA AFYA KUONGEZA WATUMISHI HOSPITALI MPYA YA WILAYA



*Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI (Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe ) Dkt.Wilson Mahera (mwenye koti) alipofika kukagua ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya ya Same,aliyeongazana nao ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba(kulia)na kushoto ni Katibu Tawala wa Wilaya Bi.Upendo Wella na Mganga Mkuu wa Wilaya Dkt. Alex Alexander.*

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe Dkt. Wilson Mahera ameahidi kuongeza watumishi kwenye Hospitali mpya ya Wilaya ili kuboresha utoaji wa huduma na pia kuipatia Wilaya ya Same magari matatu ya Idara ya Afya ili kurahisisha kazi mbalimbali zinazofanywa na Idara hiyo.

Dkt.Mahera aliyasema hayo akiwa katika ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya ya Same ambapo alisema magari yatakayotolewa ni magari mawili ya kubebea wagonjwa (ambulance) pamoja na gari moja ya matumizi ya kawaida (hardtop).

"Utaratibu wa kupatiwa gari mbili yaani ambulance moja na hardtop moja umeshakamilika na mtazipokea wakati wowote lakini ambulance moja mtasubiri kidogo"alisemaDkt.Mahera

Pia Naibu Katibu Mkuu huyo ameahidi kuiongezea Hospitali hiyo fedha kwaajili ya kumalizia awamu ya pili ya mradi huo ambayo inajumuisha umaliziaji wa ujenzi wa Jengo la Utawala, Jengo la Kufulia, Wodi za Wagonjwa na kujenga njia za kutembelea wagonjwa (walkways)

“Niwapongeze kwa kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD) katika Hospitali hii lakini niwaahidi kuwa tutaleta fedha za ukamilishaji wa Mradi huu ili majengo yote yaweze kutoa huduma na Mradi huu uweze kuwa na tija kwa wananchi” alisema.

Akitoa taarifa ya Ujenzi huo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same Dkt. Alex Alexander alimuomba Naibu Katibu Mkuu kuipatia Hospitali hiyo pamoja na Wilaya nyongeza ya Watumishi kwani Wilaya inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa Afya.

Aidha Dkt. Alex aliiomba Serikali kusaidia kujenga nyumba za Watumishi kwenye hospitali hiyo mpya ya Wilaya kwani hakuna nyumba za kupanga karibu na eneo la Hospitali.

"Tunakabiliwa pia na changamoto ya ukosefu wa uzio kwaajili ya usalama kwasababu hapa ni mapitio ya Tembo hivyo tunahitaji uzio kwaajili ya usalama wa Watumishi na Wagonjwa”alisema Dkt Alex.

Naibu Katibu Mkuu Dkt Mahera alisema Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya wa sekta ya Afya mwezi huu (Novemba 2023) hivyo Wilaya ya Same itapata mgawo.

Aidha Dkt. Mahera alisema katika kukabiliana na Upungufu mkubwa wa watumishi wa Afya hapa nchini Serikali inatarajia kuajiri wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambao ni

wahitimu wa kidato cha nne ambao watapatiwa mafunzo ya miezi sita ili waweze kusaidiakutoa huduma za afya kwa kushirikiana na madaktari na wauguzi waliopo.



*Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI (Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe) Dkt. Wilson Mahera akikagua jokofu la kuhifadhia chanjo katika Hospitali mpya ya Wilaya.*

## WAZIRI KAIRUKI AAHIDI KUCHIMBA KISIMA KIBACHA SEKONDARI




*Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki akizungumza na wahitimu wa kidato cha nne kwenye shule ya Sekondari Kibacha.*

Waziri wa Maliasili na Utaliii Mhe. Angellah Kairuki ameahidi kuchimba kisima cha maji katika shule ya Sekondari Kibacha iliyopo wilayani Same mkoani Kilimanjaro ili kutatua

changamoto ya upatikanaji wa maji katika shule hiyo.

Ahadi hiyo ya Mheshimiwa Kairuki aliitoa katika mahafali ya 17 ya kidato cha nne shuleni hapo kufuatia ombi la Wanafunzi wa shule hiyo wakati wakifanya igizo ambapo walieleza kukabiliana na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Kairuki ambaye alikuwa mgeni Rasmi katika mahafali hayo alisema kisima cha maji atakachochimba pia itakua fursa ya kilimo cha mbogamboga ili kuimarisha lishe kwa wanafunzi shuleni hapo.

Mheshimiwa Kairuki alisema Serikali imefanya kazi nyingi katika uboreshaji wa elimu ikiwemo utekelezaji wa Miradi lipa kulingana na matokeo (EP4R) ambao kwa mwaka wa fedha 2022/23 umetoa Bil.7.5 kwaajili ya maendeleo ya shule mbalimbali za sekondari hapa nchini.

"Serikali yetu kupitia mradi wa EP4R umetoa fedha zaidi ya Bil.7.5 kwaajili ya ujenzi wa mabweni, matundu ya vyoo,vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali za kidato cha tano na sita na same pia imeweza kunufaika" amesema Mhe.Kairuki.

Huku Mradi wa SEQUIP umetoa shilingi billioni 48 kwaajili ya kujenga shule za wasichana za bweni ambapo wilayani Same ni miongoni mwa wilaya zilizo nufaika na mradi huo.

"Nipende kuwapongeza sana Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa usimamizi mzuri wa Miradi,nimeona katika Shule Mpya ya Msingi Kisima ni shule nzuri imejengwa vizuri sana na Shule ya Chekechea ya mfano liyopo pale pia imejengwa vizuri,natamani Wilaya nyingine waje wajifunze hapa kwenu "alisema Kairuki.

Pia aliwaasa wahitimu hao wapatao 165 kutumia muda wao vizuri kwa kusoma kwa bidii kuongeza utiifu na nidhamu kuelekea mitihani ya Taifa.

Nae Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe. Kasilda Mgeni ameishukuru serikali kwa kuikumbuka Wilaya ya Same na kutoa fedha za miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa ujenzi wa barabara pamoja na mradi wa maji wa Mwanga- Same- Korogwe ambao Mhe. Kasilda Mgeni amesema kufikia Juni 2024 mradi huo utakua umekamilika na kuwatua ndoo kichwani wakazi wa Same

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Wilaya ya Same Bi. Anastazia Tutuba alitoa salamu za shukrani kwa Mhe.Angellah Kairuki kwa kusaidia fedha kwaajili ya shughuli mbalimbali za kimaendeleo wakati alipokuwa Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI.
"Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri maana kipindi ukiwa Waziri wa TAMISEMI

Wilaya yetu kwa mwaka jana iliweza kupokea Bil.15 kwaajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ikiwemo Ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya"alisema Tutuba.
Serikali mkoani Kilimanjaro imeahidi kuwatafutia wajasiriamali wanawake masoko ya bidhaa mbalimbali wanazozalisha ili waweze kujikimu kiuchumi.

# ‘WANANCHI TUNZENI MIUNDOMBINU YA MAJI’-RC BABU



***Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu akitoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni alipokuwa ziarani Wilayani Same.***

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu amewataka wananchi kutunza miundombinu ya maji ili iweze kudumu muda mrefu.

Mheshimiwa Babu ametoa wito huo Oktoba 27 mwaka huu wakati alipotembelea Mradi wa Maji wa Mabilioni -Kijomu.

"Wito wangu kwenu ni kuhakikisha mnatunza miundombinu ya maji ili iweze kudumu muda mrefu na kunufaisha wananchi wengi zaidi"alisema

Aidha alikitaka Chama cha watumia maji Kata ya Mabilioni kusimamia vema ukusanyaji wa michango ya maji ili iweze kuwafaa pale kunapokuwa na matengenezo madogo madogo kwenye gati za maji.

Awali akitoa taarifa ya ujenzi wa Mradi wa maji Kijomu-Mabilioni Meneja wa Ruwasa Wilaya ya Same Mhandisi Abdallah Gendaheka alisema Mradi huo umegharimu Shilingi Milioni 422.

Alisema Mradi huo umeshakamilika na unanufaisha wakazi zaidi ya elfu tano wa Kata za Mabilioni na Hedaru.

Aidha Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Babu amewataka wananchi wa Mkoa huo kutunza vyanzo vya maji pamoja na mazingira yanayowazunguka kwa kuotesha miti kwa wingi na kuepuka kufanya shughuli za kilimo karibu na vyanzo vya maji.

Amesema uharibifu wa mazingira unasababisha njaa maana misimu ya kilimo inavurugika na pia huleta ukame na hivyo kusababisha mifugo kufa kwa kukosa malisho na maji.
"Otesheni miti pembezoni mwa barabara zote,otesheni miti mingi kuzunguka vyanzo vyote vya maji ili kuhakikisha kwamba kijani ya Kilimanjaro inarudi" alisema Mheshimiwa Babu.
Amesema lengo lake ni kuhakikisha kuwa Hali ya Kijani iliyokuwa imezoeleka inarudi katika Mkoa wa Kilimanjaro.

"Ni kweli kwamba mti ni wako na umeuotesha wewe na umeutunza wewe lakini huruhusiwi kuukata bila kuwa na kibali cha Serikali "alisema Babu.

Akizungumza katika ziara hiyo Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni alimuahidi Mkuu wa Mkoa kufuatilia agizo hilo na kuhakikisha kuwa miti inaendelea kupandwa katika maeneo mbalimbali ya Wilaya hiyo.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa tumepokea maelekezo yako na tunaahidi kuendelea na jitihada za kupanda miti katika maeneo yote"alisema Mkuu wa Wilaya

Katika ziara hiyo Mkuu wa Mkoa alitembelea Shule ya Msingi Dimbwi ambapo akikagua madarasa matatu ya Mradi wa Boost, Ujenzi wa Daraja linalounganisha Kata za Bwambo na Mpinji pamoja na Uzinduzi wa Jengo la mama na mtoto la Kituo cha Afya Bwambo.

Miradi mingine aliyoitembelea ni pamoja na Ukaguzi wa ujenzi wa Shule Mpya ya Msingi ya Kisima,Ujenzi wa Hospitali Mpya ya Wilaya na Mradi wa Maji Mabilioni na Kijomu.

## ‘TUENDELEE KUCHUKUA TAHADHARI YA MAFURIKO-DED TUTUBA



***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bi. Anastazia Tutuba akizungumza katika kikao cha Ba raza la Madiwani.***

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi. Anastazia Tutuba amewataka wananchi Wilayani humo kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya mafuriko kwani mvua za Elnino bado zinaendelea.

Kwa mujibu wa Taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) mvua za Elnino zinatarajia kunyesha hadi mwishoni mwa mwezi Februari 2024.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani Mkurugenzi huyo alisema tayari Kamati za kukabiliana na maafa zimeshaundwa kuanzia ngazi ya Vitongoji,Vijiji na Kata na tayari zimeshapewa maelekezo kuhusu hatua za kuchukua pale hali inapokua ya kuhatarisha.

"Swala la majanga ya mafuriko linadhibitiwa kuanzia ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa mpaka Taifa, hivyo sisi kama Halmashauri tayari tumeunda Kamati za maafa ambazo kwa sasa zinaendelea kutoa elimu juu na namna ya kujikinga na Maafa"alisema Bi.Tutuba

Alisema katika Wilaya ya Same kuna maeneo hatarishi ambayo hata kipindi cha Mvua za kawaida za masika hukumbwa na mafuriko hivyo wananchi walishaelekezwa kuhama kwa muda katika maeneo hayo.
Aliyataka maeneo ambayo hukumbwa na adha ya mafuriko katika Wilaya ya Same kuwa ni Hedaru,Makanya,Kisima,Ruvu,Njoro na maeneo mengine ambayo hupata majanga ya maporomoko ya miamba ni Myamba,Msindo,Vunta na Mtii.

"Kwa kipindi hiki cha Mvua za Elnino ni vema wananchi wakaepuka kukaa chini ya miti, waepuke kupita na vyombo vya Moto maeneo yenye maji mengi, wasiguse nyaya za umeme popote wanapoziona,lakini wanatakiwa pia kuwa na namba za viongozi wao ili hata majanga yanapotokea waweze kutoa taarifa ili wapate msaada wa haraka" alisema.



***Wananchi wa Kata ya Hedaru wakiondoa matope kwenye maeneo yao baada ya eneo hilo kukumbwa na Mafuriko.***

# DC KASILDA ATAKA MITI INAYOOTESHWA KUTUNZWA




***Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe Kasilda Mgeni akiotesha mti kwenye eneo la Hospitali mpya ya Wilaya kama ishara ya uzinduzi wa kampeni maalum ya kuotesha miti katika Wilaya ya Same.***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni amezitaka taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali kuhakikisha kwamba miti yote inayooteshwa kipindi hiki cha mvua inastawi.

Ameyasema hayo wakati akizindua zoezi la upandaji miti kwenye Wilaya ya Same kwa msimu wa 2023/24 ambapo alisema ni vema miti yote inayooteshwa ikasimamiwa vema iweze kuota na kukua.

“Tunaotesha miti mingi sana kila mwaka lakini tujiulize katika miti tunayootesha ni mingapi inayostawi na kukua vizuri,katika eneo hili tunapaswa kuwa makini” alisema Mheshimiwa Kasilda

Mkuu huyo wa Wilaya alisema mabadiliko ya tabia nchi yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira ni makubwa mno kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu ambazo zinasababisha mitiu mingi kukatwa hivyo hatuna budi kukabiliana na hili kwa kuotesha miti kwa wingi na kuhakikisha miti hiyo inakua.

Akizungumza katika uzinduzi huo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba alisema kwa upande wa taasisi za Serikali miti yote inayooteshwa inasimamiwa vema ambapo Zaidi ya asilimia 95 ya miti inayooteshwa hukua vema.

Kila mwaka tuna lengo la kuotesha miti mil.1.5 ambapo miti hugawanywa kwenye taasisi za serikali,taasisi binafsi na kwa mtu mmojammoja kwaajili ya kuotesha na imeshaanza kuleta tija” alisema Bi.Anastazia.

Alisema katika maeneo ya shule zote za  Msingi na Sekondari zikiwemo za Serikali na binafsi zimezungukwa na miti mingi na bado wanaendelea kupewa miti ili waweze kuotesha.

Katika Uzinduzi huo jumla ya miti 1,000 ilioteshwa katika eneo linalozunguka Hospitali mpya ya Wilaya ya Same ambapo miti mingine 99,000 iligawanywa kwaajili ya kuoteshwa kwenye taasisi nyingine za serikali.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Tanzania Footmark Safaris ambao ndio waliofadhili miti hiyo Bi.Rehema Mghamba alisema wamekuwa wakishirikiana na Serikali kuotesha miti ili kuendeleza vivutio vya utalii.

“Sisi tunafanya biashara ya Utalii na unapozungumzia utalii kwa kiasi kikubwa tunamaanisha uwepo wa wanyama na viumbe hai vingine, sasa ili hivi vyote viwepo ni lazima tuendelee kuotesha miti tena kwa wingi”alisema Bi.Rehema.

Nae Afisa Misitu wa WIlaya ya Same Bw.Ally Mngwaya amesema hadi kufikia Mwezi Desemba 2023 tayari jumla ya miti 512,354 imefanikiwa kuoteshwa.

## MAADHIMISHO YA SIKU YA LISHE YAFANA-WANANCHI WAHIMIZWA KULA MLO KAMILI




***Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni (kulia),Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anasatazia Tutuba (Katikati) na Diwani wa Kata ya Ruvu Yaigongo Mrutu(kushoto) wakifuatilia maadhimisho ya siku ya Lishe.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imeadhimisha siku ya Lishe katika Wilaya hiyo kwa lengo la kuikumbusha Jamii kuzingatia mlo kamili katika kila mlo wanaokula ili kuimarisha afya zao.

Akizungumza katika maadhimisho hayo yaliyofanyika kwenye Kata ya Ruvu, Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni aliwataka wananchi kuzingatia maelekezo ya wataalam wa Lishe ili kuhakikisha kuwa wanaokula mlo ulio bora.

Mkuu wa Wilaya ambaye pia alipata fursa ya kutembelea mabanda ya maonyesho ya vyakula mbalimbali vinavyoimarisha afya aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa kuandaa siku ya lishe ambayo imewawezesha wananchi wengi kupata elimu ya Lishe.

"Hii siku ni muhimu sana kwani inaongeza uelewa wa wananchi kuhusu Lishe bora lakini nichukue nafasi hii kuwahimiza wanawake wajawazito kuhudhuria Clinic ili waweze kupata chanjo mbalimbali lakini pia watoto wote Chini ya miaka mitano wapelekwe clinic ili kujua Maendeleo ya ukuaji wao na pia waweze kupata chanjo" alisema Bi.Kasilda

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Bi.Anastazia Tutuba aliwataka wazazi wenye watoto mashuleni kuhakikisha kuwa wanachangia chakula ili watoto wao waweze kupata chakula cha mchana shuleni.

Alisema Wilaya ya Same ni miongoni mwa Wilaya zilizosaini Utekelezaji wa Mkataba wa Afua za Lishe ambapo Wanafunzi kupatiwa chakula cha mchana shuleni ni kigezo cha muhimu.

"Tumeshatunga Sheria ndogo ya Mahudhurio ya lazima shuleni na uchangiaji wa chakula shuleni sasa mzazi yeyote asiyetaka kuchangia chakula kwa hiari shuleni basi atakutana na mkono wa Sheria "alisema Bi.Tutuba.

Akizungumza katika maadhimisho hayo Afisa Lishe wa Wilaya ya Same Bi.Jackline Kilenga amesema kwa sasa Wanafunzi wanaokula shuleni ni asilimia 85 Kati ya Wanafunzi 63,512 wanaopaswa kupata chakula shuleni.

Kwa upande wa kutembelea Kaya zenye wajawazito na watoto wadogo tumefanikiwa kwa asilimia 100 ambapo Kaya 5,310 zilitembelewa,na Vijiji vyote vina utaratibu wa kuwabana wazazi na walezi juu ya masuala ya Lishe"amesema Bi.Kilenga.




***Afisa Kilimo Bi. Debora Samwel akitoa elimu ya lishe bora kwa wananchi waliohudhuria maadhimisho ya lishe yaliyofanyika kwenye Kata ya Ruvu.***

## ‘SERIKALI KUENDELEA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU’




***Madarasa yaliyojengwa na Serikali kupitia Mradi wa Sequip kwenye shule ya Sekondari Mighareni.***

Serikali inaendelea kuboresha miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari wilayani Same lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mazingira ya kujifunzia yanaimarshwa ili kuweza kuleta matokeo bora.

Hayo yameelezwa na Afisa Elimu Sekondari Wilaya ya Same Bi. Neema Lemunge wakati akizungumza kwenye Mahafali ya 28 ya kidato cha nne Shule ya Sekondari Kwizu iliyopo katika Kata ya Mshewa ambapo alisema miundombinu yote chakavu itafanyiwa ukarabati ikiwa ni pamoja na kujenga upya iwapo haitafaa kukarabati.

Amesema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24 Divisheni ya Elimu Sekondari imepokea zaidi ya shilingi Bil 3 kwaajili ya kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule mpya za Sekondari.

Katika Risala ya wanafunzi kwenye mahafali hayo walieleza changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya madarasa na vyoo vya wanafunzi.

"Naomba niwatoe shaka kwamba Ofisi ya Rais TAMISEMI tayari imechukua takwimu ya miundombinu chakavu katika shule zote za Serikali nchini ikiwemo shule hii, hivyo tunatarajia kupokea fedha kwaajili ya ukarabati na ujenzi.

Aidha Afisa Elimu Bi. Lemunge amewataka wazazi kusimamia jukumu lao muhimu la kuhakikisha watoto wanahudhuria masomo na pia wanapata mlo wa mchana wawapo shuleni.

"Ikibainika kuna wazazi wanaochangia utoro kwa watoto tutawachukulia hatua kali, lengo la serikali kutoa elimu bure ni kuhakikisha kuwa watoto wote wa kitanzania wanasoma, hivyo ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha kuwa mtoto wake anahudhuria masomo" alisema Lemunge.

Jumla ya wanafunzi 62 wamehitimu kidato cha nne shuleni hapo

Nae Diwani wa Kata ya Mshewa Mhe. Gaitan Mkwizu, amepongeza jitihada zilizofanywa na wananchi za kushiriki katika kujenga bweni la wanafunzi wa kike shuleni hapo.

" Na sasa wanakijiji tumekubaliana kuanza kujenga vyoo vya wanafunzi wakati tukisubiri msaada wa Serikali ili tuweze kukamilisha"amesema Diwani huyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Kwizu Bw.Luseko Mpokera, aliishukuru Serikali kwa kutoa fedha kwaajili ya ujenzi wa bweni  na ujenzi wa madarasa mawili ambayo tayari yamekamilika na kutumiwa na kidato cha kwanza.

"Lakini pia niishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa kutoa fedha milioni 20 ya mapato ya ndani kwaajili ya umaliziaji wa bweni hili" alishukuru Mkuu  huyo.

# WAFANYABIASHARA TUMIENI MASHINE ZA EFD-DC AONYA



***Mkuu wa Wilaya ya Same akikagua risiti ya EFD katika moja ya maduka Wilayani Same wakati alipofanya ziara ya kuhamasisha matumizi ya mashine za EFD.***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni amewataka wafanyabiashara wanaostahili kutumia mashine za EFD kuhakikisha wananunua na kutumia mashine hizo ili waweze kulipa kodi sahihi za Serikali.

Mhe.Kasilda ametoa agizo hilo baada wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua na kuhamasisha matumizi ya mashine za EFD kwenye maduka yaliyopo Same Mjini ambapo alisema wapo wafanyabiashara ambao wameshaandikiwa barua na MAmlaka ya Mapato (TRA) Wilayani humo wakitakiwa kutumia mashine hizo lakini bado hawajafanya hivyo.

Mkuu wa Wilaya alitoa mwezi mmoja kwa Wafanyabiashara wote wanaopaswa kuwa na mashine za EFD wanunue mashine hizo ili waweze kulipa kodi stahili lakini pia amewataka wale ambao wanazo mashine hizo kuhakikisha kuwa kila mteja anapatiwa risiti.

"Lengo la ziara hii ni kuhakikisha kuwa mapato ya Serikali hayapotei, kila mfanyabiashara alipe Kodi stahili ya Serikali ili kwa pamoja tuijenge nchi yetu"alisema Mkuu huyo.

Akizungumzia ziara hiyo Meneja wa TRA Wilaya ya Same Bw. Eliapenda Mwanri alisema Wilaya hiyo ina jumla ya Wafanyabiashara 1,300 waliosajiliwa TRA ambapo alisema Kati yao ni wafanyabiashara 180 ndio wanaotumia mashine za EFD.

"Wapo baadhi ya Wafanyabiashara ambao wanastahili kuwa na mashine hizo kutokana na mauzo yao na hawa tayari tumeshawaandikia barua za kuwataka kununua mashine na wazitumie"alisema Meneja huyo.

## DED SAME AWAZAWADIA WALIOFANYA VIZURI UMISHUMTA NA UMMITASETA.



***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi. Anastazia Tutuba akimkabidhi zawadi Mwalimu wa Michezo Nathaniel Msangi***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imetoa zawadi na vyeti kwa wanafunzi na Walimu waliowezesha Timu za UMISETA na UMITASHUMTA kufanya vizuri katika mashindano ya michezo kuanzia ngazi ya Wilaya , Mkoa hadi Taifa.

Akitoa zawadi kwa walimu na wanafunzi hao , Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Same Bi. Anastazia Tutuba alisema zawadi hiyo ni motisha tu kwa walimu na wanafunzi walioiwakilisha vema wilaya ya Same.

"Wakati wanaondoka kwenda kwenye mashindano niliwaambia waende wakang'ae huko na kweli wamefanya hivyo napenda kuwapa zawadi hii ya shilingi laki tano ili wakati mwingine wajitahidi zaidi na kupeperusha bendera ya Same vizuri" alisema Bi.Anastazia

Mkurugenzi huyo alisema kwa kuanzia ameamua kutoa kiasi hicho cha fedha lakini wakati mwingine Halmashauri itajipanga ili iweze kuwapongeza kwa kikubwa zaidi.

Akizungumzia mafanikio ya Timu za Wilaya ya Same katika Mashindano hayo, Kaimu Afisa Utamaduni,Sanaa na Michezo wa Wilaya ya Same Bw.Nevlin Nyange alisema kwa ngazi ya Mkoa katika michezo wa  mpira wa miguu kwa wavulana na wasichana  zilishika nafasi ya kwanza, mchezo wa wavu ilishika nafasi ya kwanza kwa wasichana na mchezo wa kikapu nafasi ya pili kwa wavulana.

Amesema mchango wa Wilaya ya Same katika kuunda timu ya Mkoa imetoa wanafunzi 29 na waalimu 2 kwa michezo ya umitashumta na umisenta ambayo ni sawa na asilimia 34.8 katika timu ya Mkoa.

"Mkoa wa Kilimanjaro umeshika nafasi ya nne kwa Tanzania bara na Visiwani na kutoa mwalimu mmoja wa kike kwa mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika nchini Rwanda hii ni hatua kubwa kwa Mkoa na Wilaya yetu ya Same" amesema

Mkoa wa Kilimanjaro kwa mashindano ya mwaka uliopita 2022 ulishika nafasi ya 6 kitaifa huku kwa mwaka huu 2023 ukishika nafasi ya 4 kitaifa ambapo Same inajivunia kuwa sehemu ya mafanikio haya ya Mkoa.

Bw. Nevlin alisema kwa sasa Wilaya inaendelea kunoa timu zake  kwaajili ya maandalizi ya mwakani ili kuusaidia Mkoa kuiendea nafasi ya pili kama sio ya kwanza Kitaifa.

## KAMATI YA FEDHA NA MIPANGO YAAGIZA UJENZI WA BWENI LA VUMARI KUKAMILIKA KWA WAKATI.



***Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Mathias Mrita akitoa maelekezo kwa fundi wakati Kamati hiyo ilipofika kukagua Ujenzi wa Bweni katika Shule ya  Sekondari Vumari.***

Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Same imeielekeza Kamati ya Ujenzi wa Bweni la Wasichana kwenye shule ya Sekondari Vumari kuhakikisha kuwa ujenzi huo unakamilika kwa wakati.

Akizungumza wakati Kamati hiyo ilipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Bweni hilo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Yusto Mapande alisema Bweni hilo linatakiwa kukamilika kwa wakati na kwa ubora unaostahili.

“Tunaona maendeleo ya ujenzi ni mazuri hivyo ongezeni bidii mmalize kwa wakati na kwa ubora ili bweni hili liweze kupokea wanafunzi kwa muda uliopangwa ”alisema Mhe.Mapande

Akitoa taarifa ya ujenzi huo kwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Mkuu wa Shule hiyo Mwl. Odilia Massawe alisema kuwa bweni hilo linajengwa na fedha toka Mradi wa SEQUIP shilingi milioni 130 na milioni 12.1 ni nguvu za wananchi.

“Shule ya Sekondari Vumari ni shule ya mchepuo wa Sayansi kwa wanafunzi wa kike ambao watachukuliwa kutoka ndani na nje ya Wilaya ya Same ,bweni hili litachukua wanafunzi 80” alisema Mkuu huyo.

Diwani wa Kata ya Vumari Mhe.John Msoffe aliishukuru Serikali kwa Miradi inayotekelezwa katika Kata yake ukiwemo Mradi huo wa Bweni, Mradi wa Zahanati ya Vumari (umekamilika) na Mradi wa madarasa saba ya BOOST(yamekamilika).

“Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza fedha za Miradi kwenye Kata ya Vumari, niseme tu wananchi wangu wataendelea kushirikiana kikamilifu na Serikali katika kutekeleza Miradi yote tutakayoletewa” alisema Mhe.Msoffe.Wajumbe wa kamati hiyo pia walitembelea na kukagua Ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya,Ujenzi wa Zahanati Vumari(Ujenzi umekamilika) na ujenzi nyumba ya walimu (2 in 1) Shule ya Sekondari Mighareni.



***Nyumba ya Walimu (2 in 1)Shule ya Sekondari Mighareni***

## MBUNGE ANNE KILANGO AOMBA TARURA SAME WAONGEZEWE BAJETI



***Mbunge wa Same Mashariki Mheshimiwa Anne Kilango akizungumza na wananchi wa Idaru***

Mbunge wa Same Mashariki Mhe.Anne Kilango Malecela ameiomba Serikali kuwaongezea fedha wakala wa barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Same ili waweze kujengadaraja la kuunganisha Kata ya Kirangare na Mpinji.

Akizungumza na wananchi wa  Kata Kirangare wakati wa kutambulisha Mradi wa Ujenzi wa Barabara  ya Idaru-Narema yenye urefu wa kilomita 7 Mheshimiwa Kilango alisema Ujenzi wa Barabara hiyo ni muhimu sana kwani utasaidia kuunganisha wananchi wa Kata ya Kirangare na masoko.

Amesema bado wananchi wa Kirangare ambao wanategemea soko la Myamba na kiwanda cha Tangawizi Myamba hawataweza kuvuka upande wa pili hadi daraja hilo litakapokuwa limejengwa.

Kwa Upande wake Meneja wa TARURA Wilaya ya Same Mhandisi James Mnene amesema barabara hiyo ya km 7 inayojengwa kwa kiwango cha changarawe inagharimu jumla ya shilingi milioni 395 ambazo ni fedha za tozo.

“Kuhusu Ujenzi wa daraja la kuunganisha Kata hizo mbili Mhandisi Mnene amesema TARURA itakokotoa gharama za Ujenzi na itaziwasilisha TARURA Mkoa kwaajili ya mapitio ili daraja hilo liweze kujengwa” alisema Mhandisi Mnene.

# HABARI KATIKA PICHA



***Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa  Angella Kairuki akiombewa dua na wazee baada ya kuwasili kwenye mahafali ya kidato cha nne kwenye shule ya Sekodari Kibacha***



***Diwani wa Viti Maalum Chome Suji Mheshimiwa Habiba Irigo akichangia hoja kwenye kikao cha Baraza la Madiwani***



***Afisa Usafi wa Mazingira na Usimamizi wa Taka Ngumu Wilaya ya Same Bi. Yuster Malisa akitambulisha Mradi wa P4R kwa Wakuu wa Idara,Vitengo na Watendaji wa Kata zilizoteuliwa kutekeleza Mradi huo Endelevu wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambao unahamasisha matumizi ya vyoo bora majumbani na shuleni,matumizi ya vifaa maalumu vya kunawia mikono majumbani na shuleni,Mradi huo katika Wilaya ya Same unatekelezwa kwenye kaya 200 kutoka vijiji 10 na umepatiwa Tsh.Mil 238 kama mbegu (kianzio) na iwapo utaonyesha mafanikio mbegu hiyo inaweza kuzaa zaidi ya Bil 1 .***



***Kaimu Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Kilimanjaro Bw.Alphonce Lekule (kulia) na Afisa Ardhi Mteule wa Wilaya ya Same Bi.Angelina Sampa wakisikiliza malalamiko ya wananchi ya Ardhi wakati 'Ardhi Clinic' inayoendeshwa na Ofisi ya Kamishna Mkoa wa Kilimanjaro ilipofika Same kwaajili ya kusikiliza kero za Ardhi na kuzipatia ufumbuzi.Katika zoezi hilo lililoendeshwa kwa siku tatu pia wananchi waliweza kupatiwa hati miliki 115 za nyumba.***



***Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI (Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe) Dkt. Wilson Mahera akiotesha mti katika eneo la Hospitali mpya ya Wilaya ya Same mara baada ya kumaliza kukagua ujenzi wa Hospitali hiyo.***




**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138,SAME**

***Mhariri wa Mkuu:Anastazia Tutuba***

***Mhariri wa Habari:Amina Sangawe***

***Desemba 2023 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***